MKULIMA WA
SEVIA

Free copy
Desemba, 2016 - Machi, 2017 #4

Uzalishaji wa mboga katika msimu wa joto (Octoba – Februari)

Mipango sahihi katika msimu huu utaleta mafanikio katika uzalishaji wa mboga mboga

Tuko katika kipindi cha mvua fupi (Oktoba mpaka Desemba), kipindi cha joto kali na mvua zisizo za uhakika na zitakazoendelea katika joto na ukame hadi kipindi cha Januari mpaka Februari. Hali ya hewa katika kipindi cha Octoba mpaka Februari ina athari katika ukuaji wa mazao, wadudu na viwango vya magonjwa. Kwa wakulima, ni vizuri kujipanga katika msimu huu.

Ni nini muhimu hasa katika msimu huu? Wakulima wengi wanahofia uhaba wa maji na joto, ambavyo wadudu wengi hupenda. Kwa sababu hii, wakulima wengi huacha kupanda mboga msimu wa mvua chache. Hii hupelekea uhaba wa mboga mboga kwenye masoko mengi na bei ya bidhaa kuwa juu. Mfano; kwa kawaida kuna uhaba mkubwa wa nyanya mwezi Desemba, Januari na Februari.

Hivyo, unaweza kufikiria kuotesha mboga mboga msimu wa joto. Kabla ya kuanza, kuna mambo muhimu ya kuzingatia:

1 Unahitaji maji mengi, hasa baada ya Desemba

Ni muhimu sana kujipanga katika msimu wa mvua.Uzalishaji wa mboga mboga unahitaji maji mengi. Kwa kuwa mvua hazitoshelezi na sio za uhakika katika msimu huu, shamba linahitajika kuwa tayari mapema ili kutumia mvua za awali. Kiwango kikubwa cha joto katika msimu huu humaanisha uhitaji mkubwa wa maji. Fanya mpango kwa ajili ya umwagiliaji. Hii inawezekana kwa njia ya kutumia mkondo, kuchimba kisima au kutumia vyanzo vingine vya maji. Hakikisha unahifadhi maji kwenye bwawa au tanki.

2 Pata taarifa kuhusu uhitaji kabla ya kuamua

Kupata mawazo kuhusu uhitaji wa masoko na bei itakayofaa kwa bidhaa zako (zikiwa tayari kwa kuvunwa), pata maelekezo ya kutosha kuhusu soko. Tumia uelewa wako lakini pia kuna huduma zinapatikana: mfano, Tanzania Horticulture Association (TAHA) huweka kumbukumbu za kila siku kuhusu masoko makubwa nchini Tanzania.

3 Chagua mazao/mbegu/aina sahihi ambayo itafaa kwa msimu huu

Mazao ya mboga mboga huja katika aina tofauti na hustawi katika mazingira tofauti. Msimu huu ni mzuri sana kwa mazao kama maboga, matikiti, nyanya, biringanya, matango na pilipili. Hata hivyo, baadhi ya mazao ya msimu wa baridi yanaweza kuoteshwa kuendana aina (hasa chotora)kwani zimeboreshwa kuvumilia joto kali, mfano kabichi. Wakulima wengine huotesha kitunguu msimu wa joto. Ingawa mazao hayata kuwa mengi kama katika msimu wa mvua za masika, bei huwa nzuri masokoni.

4 Wadudu pia wanapenda joto. Elewa madhara katika msimu huu kuhusu wadudu na magonjwa kisha chukua hatua ipasayo

Wadudu

Hali ya hewa ya joto kali huongeza matukio kama vile, wadudu kuzaliana kwa kasi. Wadudu wanyonyaji na wengine kama utitiri mwekundu, nzi weupe, chawa, nzi wa matunda, kimamba na kadhalika hupenda msimu huu pia, na wako tayari kukusababishia matatizo. Hivyo hakikisha umejipanga vizuri kukinga mazao dhidi ya wadudu.

Baadhi ya mifano ya wadudu unaweza kuwaona kwenye nyanya, pilipili au biringanya na viuatilifu vya kuwadhibiti:

Wadudu	Njia za kuwadhibiti
Kimamba	Tumia Dimethoate 40% EC, Imidacloprid, Lambdacyhalothrin kuwadhibiti
Utitiri mwekundu	Dicofol, Abamectin, Imidacloprid
Utitiri	Abamectin or Thiocylam Hydrogen Oxalate 50% w/w (Evisect)
Chawa	Spinosad (Tracer 480 SC), Malathion 25% WP or Thiocylam Hydrogen Oxolate 50% w/w (Evisect)
Nzi weupe	Tumia mitego ya njano inayonata kwa nzi weupe. Lambdacyhalothrin or Thiocylam Hydrogen oxolate 50% w/w (Evisect). Thiamethoxam (Actara 25WG)
Tuta absoluta kwenye nyanya	Dawa za kutumia kukabiliana na mayai & lava: Spinosad, Methoxyfenozide, Flubendiamide Wadudu wakubwa: Chlorpyrifos

Hakikisha unatumia mzunguko wa dawa katika msimu, kwa mfano; usitumie aina moja pekee kudhibiti wadudu, ila badilisha ili wadudu wasiizoee.

Magonjwa

Unyevu unyevu mwingi kwenye majani huuongeza magonjwa katika msimu wa mvua. Ingawa magonjwa huwa kidogo katika msimu huu ukulinganisha na msimu wa mvua nyingi bado umapaswa kuangalia yafuatayo:

- Magonjwa ya kwenye majani ya nyanya (e.g. bakajani na madoajani), pilipili hoho na biringanya, ambayo yanaweza kudhibitiwa na kuzuiwa kwa kunyunyiza sumu ya Mancozeb au Chlorothalonil na Copper.
- Ubwiru unga katika matikiti ambayo inaweza kuzuiwa kwa kutumia Sulphur, Propineb au Difenoconazole.

Baada ya kutafakari, hakikisha una uwezo wa kulima zao na kulifikia mwisho kwa mafanikio. Ilikukusaidia wewe kupanga kuanzia kuotesha mpaka kuvuna, kalenda za msimu ni ya muhimu sana. Kalenda ya msimu huandaliwa kwa kuchukua karatasi na kuchora jedwali kuhusu mazao unayotaka kupanda katika msimu kwa mfululizo, na rasilimali utakazohitaji katika tarehe maalum, kama madawa ya kuulia wadudu, mbolea, mbegu, lakini pia na wafanyakazi. Zaidi ya hayo, kalenda inajumuisha na hali ya hewa. Kalenda ni muhimu katika kutambua kipindi cha kupanda na kuvuna malipo kwa wafanyakazi na fursa za masoko. Afisa ugani wa SEVIA anaweza kukusaidia kuandaa kalenda hiiy

NANENANE: Wakulima wakifanikiwa, SEVIA hufanikiwa

Hivi karibuni SEVIA ilipata tuzo ya kwanza na ya pili kwa huduma bora waliyoitoa kipindi cha maonesho ya Nanenane, mwezi Agosti 2016, yaliyofanyika Arusha na Morogoro. Kwa Dodoma, SEVIA ilikuwa chini ya Halmashauri ya wilaya ya Kondoa. Halmashauri ya Wilaya hiyo ya Kondoa ilipata tuzo ya kwanza.

Nanenane ni maonesho ya kilimo yanayoandaliwa na TASO (Tanzania Agricultural Society Organisation) ambayo huleta kwa pamoja sekta za kilimo kutoka kwenye ulimwengu wa kilimo biashara, kwa sekta za umma za kilimo na mashirika yasiyo ya kiserikali duniani huwakutanisha maelfu ya wakulima. Kwa siku nane Agosti kila mwaka (1 Agosti - 8 Agosti) wakulima wanapata wanachohitaji kwa pamoja. Kwa hiyo si ajabu kwa SEVIA kutotaka kupoteza nafasi hiyo muhimu ili kufikia mamia ya wakulima kwa huduma za ugani. Hii sio mara ya kwanza kwa SEVIA kushiriki katika maonesho ya Nanenane. Mwaka 2015, SEVIA iliweza kufikia wakulima 271 kwa huduma za ugani kwenye maonesho yaliyofanyika Arusha na ilipata tuzo ya pili kwa huduma nzuri waliyoitoa kwa wakulima. Mwaka 2016, SEVIA, ilifanya maonesho sehemu tatu kwa kuonesha aina mbalimbali za mbegu zilizoboreshwa na teknolojia na kufikia wakulima 2,598 kwa huduma za ugani.

Bonaventura Lusaulwa akitoa ushauri kwa mkulima mmoja katika maonesho ya Nanenane Morogoro

Ladislaus Mkufya akiwaelezea wakulima faida za kuzalisha ndani ya Greenhouse kwenye maonesho ya Nanenane - Dodoma

Joseph Masethya akimsaidia mkulima kuhesabu mbegu zinazohitajika na kiwango cha mbolea itakayotumika shambani katika maonesho ya Nanenane -Arusha

Ilikuwa ni ushindi kwa wakulima na SEVIA wakulima walienda nyumbani na taarifa muhimu za uzalishaji wakati SEVIA ilipata tuzo kwa juhudi zao. **Hongera timu SEVIA!!!**

Waziri Martijn van Dam alitembelea SEVIA

Waziri wa kilimo nchini Netherlands , Mh. Martijn van Dam, alitembelea kituo cha SEVIA katika wilaya ya Hai (mkoani Kilimanjaro) tarehe 16 Juni 2016. Waziri alizikubali kazi za SEVIA hasa kwa kushirikishana maarifa na teknolojia na wakulima kama walivyoshuhudia wakulima waliokutana nae. Ushirikishaji wa gharama kama inavyoonekana nje ya 'greenhouse' (nyumba ya mimea) zilizopo SEVIA na pia umwagiliaji wa matone. Akizungumza kwa niaba ya SEVIA, Elijah Mwashayenyi (Mkurugenzi Mtendaji) SEVIA inashukuru msaada kutoka serikali ya Uholanzi katika kuchangia uboreshaji wa uzalishaji wa mboga mboga Tanzania ●

Abel Kuley ni nani?

Bw Abel Kuley ni meneja wa maendeleo ya bidhaa (product development manager) katika Afrisem, mradi wa kuzalisha mbegu chotara, wa East West Seed na Rijk Zwaan. Yeye si mgeni katika sekta hii hapa Afrika Mashariki kwani alikwisha fanya kazi katika sekta ya maua nchini Tanzania kwa miaka 13 na katika Artemisia kwa miaka mingine 5. Bw Kuley alijiunga Rijk Zwaan mwaka 2011. Rijk Zwaan ni moja ya wazalishaji wakubwa ya mbegu za mboga mboga duniani kwa ajili ya uzalishaji ndani ya 'greenhouse'. Wakulima wa Tanzania hupenda hoho za rangi.

Wakulima hujadiliana kupitia 'Whatsapp'

Pengine utampata Bw Kuley mashambani, kwani anapendelea kufanya kazi bega kwa bega na wakulima kila siku kuliko kuketi katika dawati. Anapenda kuwaonesha wakulima aina mpya za mazao na kuwapatia mafunzo ya njia bora ya kukuza mazao hayo. Hivi karibuni alianzisha kundi la Whatsapp, ambalo huliita 'njia ya kimkakati '. Huwa analionea fahari sana kundi lake: likiwa na zaidi ya wakulima 700 wanaojadili uzoefu wao, maendeleo ya hawa wakulima wa mboga mboga hunihamasisha kila siku.

Uwekezaji mdogo unaweza kuzaa mamilioni ya fedha

Kama SEVIA, Bw Kuley anajaribu kuwashawishi wakulima kulima katika eneo dogo, kwa kuonesha kuwa wanaweza kupata mavuno mazuri na mengi zaidi kwa kutumia mbinu bora za kilimo. Kwa uzoefu wa Bw Kuley, hata wakulima wa teknolojia ya juu nchini Tanzania walianzia kulima katika maeneo madogo: 'uwekezaji katika eneo dogo, kama 1/6 ya ekari kwenye uzalishaji ndani ya 'greenhouse', inakuwezesha kuvuna mamilioni ya shilingi.'

Washauri wabadilike

Kuley anakubali kwamba kilimo pia kina changamoto yake. Kwa mfano, wakati bei ikishuka, wakulima wana athirika. Alitoa mfano wa pilipili hoho za rangi, hapo mwanzo, wazalishaji wa hoho za rangi ndani ya 'greenhouse' walifanya biashara nzuri kwa sababu walikuwa wachache. Lakini sasa hivi 98% ya wakulima wa kilimo cha ndani ya 'greenhouse' Tanzania wanalima hoho za rangi, na usambazaji sokoni ni kubwa hivyo bei imeshuka.'Hata hivyo', Bw Kuley alisema,' bei haitashuka sana kama nyanya, kwa sababu hoho za rangi ni zao jipya ambalo bado linapenya katika masoko yetu ya ndani. Hali kadhalika Rijk Zwaan imeunda kalenda. Tunawashauri wakulima wetu wa kilimo cha 'greenhouse' kuzalisha nyanya kipindi cha kiangazi (Januari hadi Juni) wakati wakulima wengi wa nje hawatazalisha. Baada ya hayo, tunapendekeza wabadili na kulima hoho za rangi wakati wa mvua za masika (Aprili kwa Agosti) kwa sababu Julai, Agosti na Septemba ni miezi ya kilele cha utalii na mahitaji ya hoho za rangi huongezeka katika mahoteli.'



'Hawa wakulima wa mbogamboga wanani hamasisha kila siku'

SEVIA ni mkufunzi

Bw Kuley hufanya kazi kwa ukaribu na wataalamu wa SEVIA: 'Wakati sisi, kama wazalishaji wa mbegu, tunaendelea kukidhi mahitaji ya wakulima, SEVIA imekuwa mkono wetu wa pili baada ya kupeleka maafisa ugani nchini Tanzania, ambao hutoa mafunzo kwa wakulima kupitia maonesho ya shamba darasa. Wakulima sasa wana ufahamu zaidi wa aina za mbegu chotara na teknolojia zinazohusika wakati wa kutumia hizi mbegu ambazo zina zalisha sana japo ni za gharama.' Anasisitiza kwamba huko mbeleni wakulima lazima waweze kuhusisha SEVIA kama 'mkufunzi', kwani SEVIA imewekeza nguvu kazi yote katika kuwaelimisha wakulima na wataalamu wa sekta. 'Ni matumaini yangu kwamba SEVIA inaendelea kufikia wakulima wengi zaidi'

Mpendwa msomaji,

Kwa mara nyingine tena tunakaribia mwaka mwingine mzuri SEVIA. Mwaka 2016 ulikuwa ni mwaka wa kukuza kwa kasi, kitengo chetu cha ugani ambacho mpaka sasa kimefikia zaidi ya wakulima 12 000 katika wilaya 12 (mikoa 10).

Tunatarajia upanuzi zaidi mwaka 2017 na tunatarajia kuongeza timu yetu ugani kutoka wafanyakazi 14 hadi 19 hivyo SEVIA itakuwa katika wilaya 16. Ina maana, tutaongeza mashamba darasa yetu (yaani kushuhudia kauli mbiu yetu 'Kuona ni Kuamini') kufanikisha zaidi ya mashamba darasa 400 kwa mwaka. Upanuzi huu pia ni pamoja na kuwa na mkufunzi katika kituo cha SEVIA ili kuimarisha mafunzo yetu, usimamizi dhidi ya wadudu na magonjwa. Pamoja na mabadiliko hayo, ujumbe wetu kwa wakulima utaendelea kuwa ule ule:

- kuna haja ya kukabili uzalishaji wa mboga mboga kama biashara
- kuna haja ya kutafuta soko la mazao yako, kabla ya kuingia katika uzalishaji
- kuna haja ya kuwa chanzo cha maji cha kuaminika
- kuna haja ya kuchagua mbegu/aina bora
- kuna haja ya kutumia teknolojia bora na mbinu bunifu
- kuna haja ya kuboresha usimamizi wa mazao
- na kuna haja ya kutafuta msaada kutoka kwa maafisa ugani

Tunapoingia mwaka mpya, tutaendelea kusisitiza ujumbe huu na mengi zaidi.

Kwa kufanya hivyo tunatarajia kuendelea kukuhudumia. Kwa hiyo kuna kila sababu ya kuwa na matumaini na kutarajia mambo mazuri zaidi siku zijazo.

Kwa niaba ya wafanyakazi wote SEVIA na bodi, tungependa kukutakia Kheri ya Krismasi na mafanikio ya Mwaka Mpya!

Elijah Mwashayenyi
Mkurugenzi mtendaji, SEVIA

Agenda

JANUARI

- Maafisa ugani wapya wata tawanywa mikoani
- Mafunzo kwa wakulima
- Mafunzo kwa wataalamu wa kilimo
- Siku za maonesho ya shamba darasa mikoani

FEBRUARI

- Kikao cha awali cha uangalizi na ufuatiliji wa mradi wa SEVIA
- Mafunzo kwa wakulima
- Siku za maonesho ya shamba darasa katika kituo cha SEVIA

MACHI

- Mafunzo kwa wakulima
- Uchaguzi wa wakulima kwa ajili ya msimu wa mvua za masika

Stories from the field

Kuwa na 'greenhouse' (nyumba ya mimea) haikufanyi wewe kuwa mkulima mzuri, lakini kujua jinsi ya kulima ndani ya 'greenhouse' (nyumba ya mimea) ndio kutakufanya wewe kuwa mkulima mzuri. Christopher Elias Mrecha ni mkulima wa kawaida katika wilaya ya Hai ambaye alijenga 'greenhouse' kwa matumaini ya kuongeza mazao na mapato. Hata hivyo , wakati watu wa SEVIA, Tyrrel Chisenga na Epaphras Milambwe walivyomtembelea kwa mara ya kwanza, alikuwa ameotesha sukuma wiki kwenye 'greenhouse' yake.

yakiharibika. Alishajaribu kuotesha nyanya na matango na kushindwa. Ndipo alipoamua kuotesha 'Sukuma wiki'. Baada ya miaka mitatu ya kupotoka, Bw Mrecha aliamua kuwa ni alipoamua; sasa ni muda wa kuchukua hatua muhimu na kutafuta maoni kutoka kwa wataalam, ili kuongeza kiwango cha uzalishaji na kipato. Alipata habari za mradi wa SEVIA kutoka kwa Abel Kuley wa RijkZwaan alipoenda kutafuta mbegu bora. Bw Mrecha alifanya maamuzi ya haraka kutembelea shamba la SEVIA. Baada ya kutembelea kwa

Bw Mrecha alisema kwamba mara nyingi alipotoshwa kwa ushauri kuhusiana na mazao yake katika greenhouse yalikuwa

mara ya kwanza alitahadharishwa juu ya uwepo wa tatizo kubwa la ugonjwa wa mnyauko katika shamba lake. Pia ni kwa sababu ya ujenzi dhaifu wa green house, mzunguko wa hewa haukuwa wa fanisi, hivyo kusababisha magojwa mengine kutokana na unyevu wa hali ya juu

Shamba darasa la matango lilianzishwa mara moja chini ya uangalizi wa Florah Yangole na Theophilo Nyigaga, kumfundisha Bw Mrecha jinsi ya kutunza matango nje na ndani ya greenhouse. Baada ya mwezi mmoja wa mwongozo na mazoezi mazuri ya kilimo zao lake lilikuwa tayari kwa kuvunwa. Alishauriwa kutafuta soko kabla ya kuvuna. Alifanikiwa kupata soko Nakumatt Supermarket-Moshi. Kutokana na uborai wa mazao yake walimuuliza kama ataweza kuwasambazia aina zingine za mboga.

Bw Mrecha ni mmoja wa wakulima wengi wanaotumia greenhouse (nyumba ya mimea) ambao walidhani kuwa na greenhouse kutaongeza fedha mifukoni mwao. Hata hivyo, kitu kimoja wakulima wanatakiwa kutambua ni kwamba wanatakiwa kutafuta ushauri kabla na baada ya kutengeneza greenhouse. Cha muhimu ni maarifa katika kilimo!

People @ Sevia

Kutana na timu mabwana shamba wetu

SEVIA kwa sasa imeajiri mabwana shamba (maafisa ugani) 12 katika mikoa 10. Kila afisa ugani anafanya kazi na wakulima kwa kuandaa mafunzo au shamba darasa juu ya uzalishaji wa mbogamboga katika wilaya husika. Mafunzo hayo ni pamoja na matumizi sahihi ya aina za mbegu bora na teknolojia bunifu. Mafunzo, ushauri, ziara shambani na maandalizi ya shamba darasa ni sehemu na moja wapo ya kazi za maafisa ugani. Huduma yetu ni bure. Timu hii inaungwa mkono na Epaphras Milambwe (Meneja ugani) na Thobias Mkamate (Afisa ugani mwandamizi). Onana na afisa ugani wetu, huwezi jua pengine anaishi au ameweka shamba darasa karibu na wewe.

Adam Lazaro
Lushoto, Tanga
0676962801

Bonaventura Lusaulwa
Morogoro, Morogoro
0718155578 /
0763261160



Frank Mazengo
Rungwe, Mbeya
0766116117 /
0717120503

Harry Nassary
Ilemela, Mwanza
0767966646 /
0682570907

Iddi Haridi Mohamed
Meru, Arusha
0759922889

Joseph Masethya
Arusha, Arusha
0783861886

Ladislaus Mkufya
Babati, Manyara
0754727226

Lewis Mlekwa
Moshi Rural,
Kilimanjaro
0718336863

Norbeth Poncian
Kilolo, Iringa
0685942364

Nurdin Nassary
Mndoholele
Bagamoyo, Pwani
0688191820

Paschal Lusolela
Hai, Kilimanjaro
0753564741

Theophilo Nyigaga
Hai - Lambo, Mferejini
On Station
0757175288

Thobias Mkamate
Dodoma, Dodoma
0757680800

MKULIMA WA SEVIA

Wachangiaji

SEVIA, P.O. Box 7211, Moshi

Anuani ya kutembelea
Lambo, Mferejini
Tanzania
+255 685 942 364
www.sevia.biz

Michango ya jarida hili ni kutoka kwa
Epaphras Milambwe [2]
Clara Mlozi [2]
Elijah Mwashayenyi [2]
Herman de Putter [1]
Anita van Stel [3]

Wahariri
Clara Mlozi
Anita van Stel

Ubunifu
Mooizo Design

[1] Wageningen UR [2] SEVIA [3] Communications consultant

Je, unataka kupokea nakala za bure za awali za jarida hili? Tafadhali tuma barua pepe au soma jarida katika tovuti yetu www.sevia.biz